



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:

Tel: +255 262 965732 (Direct line)

+255 659 566703

e-mail: ded@sikongedc.go.tz

Tovuti: sikongedc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

4 Mtaa wa Bomani

S.L.P 70

45382 - SIKONGE TABORA

7/06/2023

TANGAZO

LA


KUTOA HUDUMA YA USAFI KWENYE OFISI ZA HALMASHAURI

LGA/121/2023/2024/NC/02

1. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inapenda kuwatangazia wananchi wote wenye Vikundi au Makampuni yenye nia na uwezo wa kutoa huduma ya Usafi katika Ofisi za Halmashauri na maeneo mbalimbali yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Kazi hii ni kuanzia tarehe 01 Julai, 2023 hadi tarehe 30 Juni, 2024.
2. Unakaribishwa kuleta Kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II.
3. Vitabu vya Kotesheni vinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa bei ya Tsh. 30,000/ kwa Vikundi au Kampuni itakayomba kazi hii
4. Kotesheni zote zitumwe zikiwa zimejazwa nakala halisi (ORIGINAL MOJA) na nakala (COPY MBILI) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa;

"KOTESHENI NA. LGA/121/2023 – 2024 /NC/02" KWA UTOAJI WA HUDUMA YA USAFI KATIKA OFISI NA MAENEO MBALIMBALI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

5. Maombi yote yapelekwe (yatumwe) kwa **Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, S.L.P 70, SIKONGE.**
6. Kikundi au Kampuni iwe na Leseni halali ya Biashara na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
7. Kikundi au Kampuni ionyeshe utambulisho kwamba inalipa Kodi (TIN Number) na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
8. Kikundi au Kampuni iwe imesajiliwa na Msajili wa Makampuni na kivuli cha usajili kiambatanishwe kwenye maombi yake
9. Kikundi au Kampuni ionyeshe uzoefu wa Kazi husika
10. Kikundi au Kampuni ionyeshe kiasi cha fedha atakacholipwa na Halmashauri kwa kila Mwezi.
11. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni **siku ya Jumanne tarehe 20.06.2023 saa 5:00 Asubuhi.** Kotesheni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya waombaji au wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.
12. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.


Seleman Pandawe
Mkurugenzi Mtendaji (W)
SIKONGE

MKURUGENZI MTENDAJI
WILAYA - SIKONGE